Vita vya Kiroho na Wewe

Na *James R Henderson Superintendent Grace Communion Europe*

Rita alikuwa amechanganyikiwa. Alikuwa muumini kwa muda wa zaidi ya miaka mitatu, na sasa kiongozi mashuhuri wa kanisa alimwambia kwamba alikuwa na pepo. Ni lazima angewekwa huru. Shetani alikuwa amemshika mkononi mwake, akasema kiongozi wa kanisa, na huenda ikawa alikuwa mmiliki wa laana kutoka kwa mababu zake.

Kiongozi wa kanisa alimwambia Rita kwamba angehudhuria mkutano wa maombi ya usiku kucha Jumapili iliyofuata kuanzia saa mbili jioni, basi angewekwa huru kutoka "utumwa wa mapepo." Rita alijua kwamba alimpenda Yesu, na pia alimwamini kiongozi wa kanisa. Je, afanye nini? Kweli, mlikuwa na pepo ndani ya roho yake akiwa mkristo?

Johana alikuwa mshiriki kanisani kwa muda wa zaidi ya miaka 10. Kanisa aliyoshiriki ilikuwa imepitia kwenye milima na mabonde kwa hali ya mwotisha, lakini yeye alikuwa ametosheka aliko. Mhubiri mgeni alikuwa amehubiri ujumbe wa kusisimua kuhusu uinjilisti, na alisema ni lazima injili isikizwe duniani kote kabla wakati haujakwisha. "Ni lazima tuwe na mpango wa maana wa kuwafikia watu wote wa kijiji, na pia duniani kote."

Yohana alikuwa amechangamka. Mhubiri alisema kweli – injili ni lazima ihubiriwe. Johana akafanya uamuzi wa kuwa mwanajeshi wa maombi kwa ajili ya uinjilisti, na akaanza kuhudhuria mikutano ya maombi ya pamoja na madhehebu mengine. Katika mojawapo ya mikutano hiyo, akafundishwa kwamba mbinu moja ya kuhubiri injili duniani kote ni kumshinda shetani na kubomoa ngome zake za kiroho. Yohana akaambiwa kwamba mapepo hutawala juu ya nchi mbali mbali, miji yao, na pia vijiji vyao. Akaambiwa kwamba mapepo hayo ni lazima watafutwe na watupiliwe mbali ili kazi ya injili iweze kufanyika. Yohana aliyawaza mafundisho hayo, lakini akaona huenda ikawa ni ya kuaminika. Kusema kweli, Shetani lazima ashindwe kabla ya injili itangazwe. Lakini Yohana alikosa uhakika – aendelee na ushirika wake na kundi hilo, ama atoke aachane nao?

Kuwekwa huru. Kuvunjavunja ufungwa. Kufunga laana. Kuporomosha ngome za kishetani. Haya ni mawazo yanayo fikiriwa sana na wakristo siku hizi. Wanatheologia mashuhuri na watu, waume kwa wanawake, wanafundisha mambo haya, na kuyahimiza. Lakini, Je, kuna usalama hapo? Je, kuna mitego kwa mambo haya?

Ukitembelea duka la vitabu ambalo liko karibu nawe, utapata kwamba vitabu vilivyopata umaarufu kwa mauzo vinahusika na swala la vita vya kiroho. Kunazo hata kanda na video kuhusu swala hili. Je, muumini afanye nini? Je, ni jinsi gani mtu, awe mume au mke, atakavyo shauriwa kuhusu mambo haya, huku baadhi ya mafundisho hayo yakiwa kinyume na mengine, kisha aweze kufika kwenye mtazamo ulio sawa sawa, na ambao unaweza kuthibitishwa kutumia Biblia?

Biblia inafundisha wazi kwamba, kunayo vita ya kiroho. Soma 1 Petero 5:8 na Waefeso 6:12. Vipengele hivi vinafundisha kwamba shetani anaendeleza vita dhidi ya bidii ya wakristo ili aipinge kazi yao ya kueneza injili. Pamoja no hayo, Biblia inaeleza kwamba kupitia kwa Kristo kuna ushindi dhidi ya vita hiyo. Ushindi tumepata tayari! (Wakolosai 1:13, Matendo ya mitume 26:18, 1 Wakorintho 15:57, Warumi 8:37-38). Kuna msingi dhabiti wa mafundisho kwa Biblia ya kwamba tuna ushindi tayari ndani ya Kristo.

Yafuatayo ni maswali sita ambayo unafaa ujiulize unapokutana na mafundisho kuhusu swala la vita ya kiroho.

JE, FUNDISHO HILO AMA ZOEZI HILO LINASHIKILIA MTAZAMO KUWA DUNIA IMEGAWANYIKA MARA MBILI?

Mtazamo kuwa dunia imegawanyika mara mbili ni wazo linaloshikilia kwamba kunazo nguvu aina mbili ulimwenguni – wema na uovu, Mungu na Shetani.

Nguvu hizi huwa katika hali ya mashindano, na wakati wo wote mshindi hajulikani wazi. Mara nyingine wema hushinda, mara nyingine uovu hushinda. Ukiangalia duniani leo, kuna watu ambao watasema kwamba uovu umeshinda vita hiyo tayari. Lakini, mtazamo wa Biblia ni kwamba Kristo amenyakua ushindi tayari, na akaushinda ulimwengu (Yohana 16:33) na kwamba Shetani tayari ameshindwa (Luka 4:1-13, Waebrania 2:14, Wakolosai 2:15).

Kweli ni kwamba "**Bwana Mungu wetu mwenyezi anamiliki**" (Ufunuo 19:6). Shetani na mapepo wanaweza kutenda lakini ndani ya mipaka iliyowekwa na Mungu. Hadithi nyingi, kama ile ya Ayubu, inaonyesha hivyo. Mtazamo kwamba dunia imegawanyika mara mbili sio ukweli wa mambo yalivyo. Mtazamo huo ni uongo wa Shetani, ambaye mapenzi yake ni "**kuwa kama yeye aliye juu sana**" (Isaya 14:14).

Mafundisho yo yote kuhusu vita vya kiroho ambayo, moja kwa moja au kwa njia ndefu, yanashikilia kugawanyika mara mbili kwa dunia hayawezi kamwe kuthibitishwa kwa Biblia, na kwa hivyo, ni ya kushukiwa.

Ushindi tumepata. Mungu ni mkuu kumshinda Shetani.

JE, FUNDISHO HILO AMA ZOEZI HILO LINAMWELEKEZA MKRISTO KUABUDU VIUMBE AMA USHIRIKINA?

Neno linalotafsiriwa “kuabudu viumbe” ni neno la Ki-Latini “anima,” ambalo lina maana ya kupumua au roho. Ni mtazamo unaoshikilia kwamba kunako duniani pepo wema na pepo wabaya ndani ya kila kiumbe, na inampasa binadamu atafute namna ya kutumia nguvu za pepo hao kwa faida yake binafsi. Tabia hii ya kuabudu viumbe inapatikana katika dini za kiasili na pia katika mfumo wa Enzi Mpya, au kwa kiingereza “New Age.”

Kudhibiti ulimwengu wa roho ndio wazo linaloarifu utumizi wa uchawi na ushirikina. Wachawi hujaribu kuwasiliana na pepo kwa njia ya tambiko, semi za kishirikina, na mbinu zingine za ufalme wa giza. Kutegemea tambiko ili kutekeleza mamlaka ni kuweka imani kwa ushirikina.

Mawazo haya ya kutumia nguvu za pepo wa viumbe vya dunia unaonekana kutumiwa na baadhi ya wakristo. Nguvu kama zile za uchawi zinatumiwa kutaja semi kama vile ‘katika jina la Yesu.’ ‘Katika jina la Yesu’ sio msemo wa kimuujiza, lakini ni msemo wa kumtambua Yesu Kristo kama Mpatinishi wetu, na kwamba kwa neema yake tumepata uhuru dhidi ya kifungo cha woga na fikira potovu.

Watu wengine watajaribu kuamuru au kufunga pepo, ambayo ni kudhibiti na kufanyiza ulimwengu wa pepo. Katika Yakobo 4:7 na 1 Petero 5:9, tunaelezwa kwamba mkristo anafaa kumjibu Shetani kwa kumpinga, wala sio kwa kumtupa nje au kumfunga mara kwa mara. Hakuna ushahidi wo wote katika Agano Jipya kwamba Mitume wa Kristo waliandaa safari ya “kutafuta na kuangamiza” pepo. Kuna wakati mara kwa mara walikutana na matendo ya pepo kwa namna iliyobidi wachukue hatua. Walipokutana na pepo, basi walishughulika nao, huku wakati wote wakiamwangazia Yesu. Lakini, Mitume hawakuenda wakitafuta pepo ili wapigane nao na kutafuta shida. Wala msingi wa huduma haukuwa uwezo wa kukemea pepo katika jina la Yesu, bali ilikuwa ni furaha ipatikanayo kwa uhakika wa kuokolewa (Luka 10:20).

Shida moja ya mfumo wa “kuwekwa huru” ni kwamba wakristo wana mwelekeo wa kuwaza zaidi jinsi Shetani anavyohusika au kutohusika na wao. Kwa njia ya kutofahamu wanaelekeza kila shida kuwa ni kazi ya shetani, na hivyo inakuwa hali ya ushirikina. Tuna ambiwa katika waraka kwa Wafilipi kwamba tuyafikirie mambo yaliyo mema na ya kutusaidia, wala sio mambo yaliyo kinyume. Tunapaswa kushughulikia uhusiano mwema na Yesu Kristo, wala sio kuwaza kila mara uhusiano wetu na Shetani.

JE, FUNDISHO HILO AU ZOEZI HILO LINASHIKILIA KUWA MKRISTO ANAWEZA KUWA NA PEPO?

Baadhi ya waumini wa kiinjilisti watasema kwamba inawezekana kwamba Kristo atadumu pamoja na pepo ndani ya muumini. Kwa kweli, wengine watasema kwamba 85% ya wakristo wana pepo ndani yao!

Fundisho hilo ni la kutisha na halina matunda ya amani. Msichana mmoja alikuja kwangu muda mfupi tu baada ya kubatizwa na kuniuliza jambo hili. Aliambiwa kwamba hata kama alipokea Roho wa Mungu, alikuwa pia na pepo kiasi fulani. Alijawa na woga mwingi, na akawa na machozi. Nilimweleza kwamba asiwe na hofu kwa sababu haiwezekani Mungu na Shetani kuishi mmoja kando ya mwingine ndani ya mkristo. **"Maana Mungu hakutupa roho ya woga, bali roho ya nguvu, ya upendo na ya moyo wa kiasi"** (2 Timotheo 1:7).

Biblia haijabainisha wazo kwamba pepo wanaishi pamoja na Kristo ndani ya muumini. 1 Yohana 5:18 inatupa moyo kwa kueleza kwamba sisi wakristo hatuguzwi na yule muovu. 2 Wathesalonike 3:3 pia hutukumbusha kwamba Yesu hutuhifadhi kutoka kwa uovu na kwamba tuna imani kuwa Mungu hutenda hivi, kama tunavyohimizwa katika Ombi la Bwana – "**bali utuokoe kutoka kwa yule muovu**" (Matthew 6:13).

Tunaweza kuwa na imani na ahadi za Mungu, kwamba tumewekwa huru, kwa njia ya msalaba, kutoka kwa nguvu za giza, na kwamba Yesu mwenyewe hutuokoa kutoka kwa uovu. Tuko mikononi ya amani. Hatuna haja ya kutegemea maneno ya kishirikina kwa mfano wa kikristo, na tabia ya kuinua mikono huku na kule, na kukemea kwa sauti kubwa pepo waliopo na wasiopo.

Furaha ya kuokolewa ni kwamba "Kristo anaishi ndani yetu" (Wagalatia 2:20, Waefeso 3:17, Yohana 17:21-23). Biblia kamwe haitufundishi kwamba Mwokozi wetu na Adui wetu wanaishi pamoja ndani yetu. Shetani haishi ndani ya muumini: Yesu huishi ndani yetu. Pepo watajaribu kutusumbua, kutujaribu, lakini hawawezi kututawala. Kuna njia moja tu ambayo pepo anaweza kuishi ndani ya mkristo: Mkristo mwenyewe akijipeana kwa huyo pepo.

JE, FUNDISHO HILO AU ZOEZI HILO LINAENDELEZA MTAZAMO BANDIA WA ROHO MTAKATIFU?

Ni wazi katika Biblia kwamba Roho Mtakatifu, aliye nafsi ya tatu kwa Utatu Mtakatifu, ni Mungu. Roho Mtakatifu sio tu malaika mwema au nguvu fulani itokayo kwa Mungu. Roho Mtakatifu ni Mungu.

Kwa bahati mbaya, baadhi ya wanaoshiriki wa vita vya kiroho humchukua Roho Mtakatifu kama malaika mwenye nguvu, au kama pepo. Tunajua kupitia Warumi 8:15 ya kwamba Roho Mtakatifu sio roho wa ufungwa, bali ni roho wa uhuru, na Yohana 14:16-17 inaeleza kwamba Roho Mtakatifu hudumu ndani ya muumini.

Pepo wanapoishi ndani ya mtu mara kwa mara huingia na kutoka wapendavyo. Lakini, Roho Mtakatifu hafanyi hivyo. Mara tu tukimpokea Roho Mtakatifu, yeye hudumu ndani yetu, na 1 Yohana 3:27 inaeleza kwamba upako ambao tunapokea tunapomkubali Yesu Kristo, hudumu nasi.

Hatari nyingine ni kumwona Roho Mtakatifu kama chombo cha kuthibiti. Roho Mtakatifu hachukui mamlaka juu ya fikira zetu na kutuelekeza kinyume na mapenzi yetu. Mungu hajatupa uhuru wa uamuzi ili tena atupokonye huo uhuru. Shetani ndiye anataka kuchukua uhuru wetu wa uamuzi. Kutamani kwetu kunyenyekea kwa Mungu wetu ni kwa hiari, si kwa lazima. Waandishi wengine wanafundisha kwamba tunaweza kumwomba Roho Mtakatifu aje na atutawale na kutufanyiza kwa lazima ili tuweze kutenda mapenzi yake. Lakini mojawapo ya tunda la Roho aishiye ndani yetu ni kiasi (Wagalatia 5:23, 1 Wakorintho 14:23). Tunda moja la kuingiwa na Shetani ni kukosa kiasi (Matendo ya Mitume 19:16).

Roho Mtakatifu hana tabia ya pepo, na hivyo fundisho lo lote ambalo linamlinganisha na tabia kama hiyo ni fundisho potovu.

JE, FUNDISHO HILO AU ZOEZI HILO LINAWEKA UZOEFU MBELE YA MAANDIKO?

Watu wengine huweka uzoefu wao kwa mambo ya kiroho mbele ya mafunzo ya maandiko. Watatetea msimamo wao kwa dhati. “Sijali usemayo, ninao uzoefu wa kiroho na uzoefu wangu una uzito zaidi ya maandiko yote utakayorusha kwangu.”

Je, shida ya mtazamo huo ni nini?

Muda fulani uliopita nilihudhuria semina ya ndoa. Mzee mmoja hapo alikuwa na shida na mkewe (kwa maoni yake!) -- alidai kwamba mkewe hakuweza kumtosheleza kwa mambo ya ngono, na hivyo akawa anamdhihaki mkewe, (na hivyo kudai kwamba mkewe ndiye mwenye makosa – jinsi tunavyojidanganya!). Ushauri aliyopewa na mshauri wa ndoa ni kwamba atafute ushirika wa ngono na mke mwingine. “Tafuta kutoshelezwa huko nje, ili uweze kuboresha ushirika wako na mke wako,” ndivyo aliambiwa. Baadaye, mtu huyo alitafuta mke mwingine, na hapo baadaye hakumdhihaki mkewe, au kumtusi. Je, hiyo ina maana kwamba uzinzi ni jambo nzuri? Hiyo ina maana kwamba uzoefu huo ni wa maana kushinda mafundisho ya maandiko? Uzoefu una nguvu kushinda maandiko?

Shida ni msemo wa hesabu ufuatao: Uzoefu = mambo yalivyo = kweli. Kwa mkristo, kweli haitegemei mambo yalivyo, au uzoefu. Hii ndio sababu tunahitaji imani. Mambo yalivyo yanaweza kutufunza kweli ya Biblia, lakini uzoefu sio msingi wa kweli. Yohana 17:17 inaeleza **"Neno lako ni kweli**." Sababu yako ya kukataa wazo ambalo linapatikana kwenye hadithi ambayo tumesoma ni kwamba unajua Biblia ina mamlaka zaidi juu ya kweli ya kimaadili. Biblia pia ina mamlaka zaidi juu ya kweli ya kiroho.

Mafundisho batili na dini za uongo mara nyingi huwa yamejengwa juu ya maono na uzoefu wa kiroho wa manabii, waume kwa wake, waanzilishi. Uzoefu wo wote – wa kimwili, wa kimawazo, wa hisia, na wa kiroho – yapasa yaangaliwe kwa mwanga wa Neno la Mungu. Jihadhari sana unaposikia mtu akisema kwamba uzoefu wake ni sawa na, au hata ni wa dhamana ya juu, kushinda maandiko.

JE, FUNDISHO HILO AU ZOEZI HILO LINADHIBITISHWA KWA MAANDIKO?

Jibu la swali hili ni wazi. Angalia ndani ya Biblia walivyofanya waBereya "**waone kwamba mambo hayo ndivyo yalivyo**" (Matendo ya Mitume 17:11).

Mafundisho mengi na uzoefu (fundisho halikubaliani na uzoefu kila wakati!) kwa swala hili la vita vya kiroho hayakubaliki kwa Biblia. Baadhi ya mafundisho huweka fundisho la Biblia kando, na wengine huenda kinyume na roho ya neema, na wengine pia huwa yanaiga theologia za kipagani.

Mafundisho potovu katika mambo haya sio kusema kwamba hakuna vita ya kiroho. Vita iko. Ushindi tunao tayari kutoka kwa mwenyezi mungu, lakini Shetani na pepo wafuasi wake maelfu, wamekata kauli kutuvamia. Tunaweza kukubaliana na maneno ya faraja yaliyonenwa na Yahazieli kwa Yehoshaphati na kwa watu wa Yudah – **"Msiogope, wala kufa moyo kwa ajili ya wingi wa watu, kwa sababu vita siyo yenu, bali ni ya mungu**" (Mambo ya Nyakati 20:15).

Yakobo anatwambia **"nyenyekea kwa Mungu. Mpinge Shetani naye atakutoroka"** (James 4:7), naye Petero anatushauri kupingana na Shetani, na pamoja na hiyo tusiwe wahukumu wa wengine, na tuelewe kwamba majaribu na shida ni mambo ya kawaida kwa wanadamu wote (I Peter 5:9).

Paulo anaeleza katika Waefeso 6:12 --18 ya kwamba vita tunayopigana ni dhidi ya uovu wa kiroho na dhidi ya "**falme na mamlaka**." Akitumia maneno yale yale ya kiyunani, Paulo anasema pia katika Wakolosai 2:15 kwamba kwa kupitia kusulubishwa na kufufuka kwa Mwokozi wetu "**akisha kuzivua enzi na mamlaka . . . akizishangilia.**" Anafurahia kwamba **"katika mambo haya yote sisi ni zaidi ya washindi kwake Yeye aliyetupenda . . . kwa maana nimekwisha kujua hakika ya kwamba, wala mauti, wala uzima, wala malaika, wala wenye mamlaka . . .**

hakitaweza kututenga na upendo wa Mungu ulio katika Kristo Yesu Bwana wetu." (Warumi 8:37 – 39).

Paulo anaendelea kusema katika sehemu ile ile ya Waefeso ya kwamba ili **"kustahimili katika siku ya uovu"** ni lazima tuvae silaha zote za mungu, na hivyo kunyenyekea mbele Yake kama alivyosema Yakobo. Tuna wajibu wa kufanya. Ni kama vile Mithali 21:31 – **"Farasi ametayarishwa kwa vita, lakini ukombozi wetu ni wa Bwana."**

Hakuna cha kuogopa. Tunao ushindi. Mungu yuko upande wa Wakristo, na "**Mungu akiwapo upande wetu, ni nani aliye juu yetu?**" (Warumi 8:31).